38:1-42:17 JIBU LA MUNGU

Utawala wa ulimwengu (38:1-38)

Labda ilikuwa mvua kali yenye radi iliyokaribia ambayo ilimsukuma Elihu atoe sifa kwa Mungu Mwumbaji kwa njia ya mashairi (taz.36:27-37:5). Ikiwa hivyo, mvua hiyo wakati huo ilishuka, na kwa ngurumo yake sauti ya Mungu ilisema na Ayubu. Mara kadhaa Ayubu alikuwa amemwita Mungu ashindane naye kwa majadiliano. Wakati huo Mungu alikubali (38:1-3).

Katika jibu lake, Mungu anamwuliza Ayubu maswali asiyoweza kuyajibu, ili amwonyeshe jinsi anavyojua kidogo tu kuhusu kazi za Mwenyezi Mungu. Mungu anaanza maswali yake ya kumchokoza, akimwuliza kwa njia ya mashairi yanayoeleza kazi zake za uumbaji wa ulimwengu zamani sana kabla Ayubu au kiumbe kingine hakijakuwepo. Malaika tu walishuhudia kazi zake (4-7). Mungu alitenga maji ya angani na yale ya duniani na kusababisha nchi kavu itokee (8-11).

Mungu anamwuliza Ayubu kama anaweza kusababisha jua liche asubuhi, ili watu wanaotegemea giza kwa kusudi la kufanya maovu 'wakung 'utwe' katika maficho yao kama vile wadudu wanavyokung'utwa kutoka nguo (12-13). Je, Ayubu anaweza kutumia miali ya jua la asubuhi ili kuchora picha nzuri za rangi mbalimbali katika sura ya dunia (14-15)? Alishuka mpaka vilindi vya bahari au alifika katika miisho ya dunia? Anajua jua linapokaa usiku, ili aweze kulisababisha lionekane asubuhi na kulipeleka mahali pa kupumzika kwake usiku? Akiwa na ujuzi mkubwa kama anavyojidai, lazima aweze kufanya mambo hayo (16-21)!

Je, Ayubu anajua jinsi Mungu anavyotawala hali ya hewa (22-24)? Ni nani atengenezaye theluji, mvua, mvua ya mawe, upepo na radi (25-30)? Anaweza kutawala na kuongoza nyota na sayari (31-33)? Anaweza kuleta mafuriko ya maji na kusababisha ukame kama anataka (34-38)?

Utawala wa wanyama wote (38:39-39:30)

Ayubu anahangaishwa zaidi Mungu anapoendelea kumwuliza maswali asiyoweza kuyajibu. Akiacha mbali ulimwengu wa kawaida, Mungu anaendelea na habari za wanyama. Anavuta mawazo ya Ayubu kwa wanyama ambao mara nyingine wanaonekana kama hawana maana kwa faida ya wanadamu, lakini ni sehemu ya mpango wa Mungu kuhusu kanuni za ulimwengu.

Mungu anamwuliza Ayubu kama anaweza kupanga kanuni za ulimwengu ili wanyama wa porini wawe na chakula chao (39-41), ambapo wanyama wa kufugwa wanatunzwa katika kuzaana kwao na kuhifadhiwa aina zao (39:1-4). Mungu ametoa uhuru kwa punda-milia na punda-mwitu, lakini wakati huo huo anatawala wanyama hao kadiri ya kanuni zake za ulimwengu. Je, Ayubu anaweza hayo (5-8)? Au anaweza kumzoesha nyati afanye kazi kama fahali au tabia ng'ombe, iwapo Mungu alimpa nyati isiyokubali kufugwa (9-12)?

Mambo mengine katika uumbaji wa Mungu yanawahangaisha watu. Kwa mfano, inaonekana kama mbuni anadharau mayai yake wala hajali vifaranga vyake, kwa sababu akitishwa anatoroka na kuwaacha peke yao. Inawezekana mwanadamu haelewi matendo ya wanyama, lakini Mungu amempa kila mnyama uwezo wake wa pekee kwa kadiri alivyoona vema (13-18). Mungu alimpa farasi uwezo wa kufundishwa. Jambo hili Ayubu anafundishwa kwa maelezo ya farasi wa vita wanaotisha sana katika mashambulio yao (19-25).

Mwewe na tai, ingawa wanajenga viota vyao sehemu za juu kuliko ndege wengine, hawana shida ya kupata chakula chao, kwa sababu macho yao ni makali mno, na hivyo wanaweza kuona vitu vidogo sana kutoka mbali. Je, Ayubu anaweza kushindana na Mwumbaji aliyepanga na kuangalia mambo hayo yote tangu mwanzo, hata yaliyo madogo sana (26-30)?

Mungu amwita Ayubu kwa majadiliano (40:1-14)

Wakati huo Mungu anamwita Ayubu ili alete hoja zake (40:1-2). Ingawa hotuba ya Mungu haikugusa matatizo ya mateso ya Ayubu moja kwa moja, si kwa kujibu maswali yake ya kiakili, wala si kwa kuthibitisha au kukanusha maneno ya marafiki zake, Ayubu hana jibu. Mungu hakumlaumu Ayubu, lakini alimwonyesha kwamba binadamu hawezi kutazamia kuelewa kila jambo kuhusu kazi ya Mungu katika ulimwengu wake mkubwa alioumba. Ayubu anasikitika juu ya maneno yake ya kwanza yenye ukali wala hana neno la kusema tena (3-5).

Lakini Mungu hajamaliza maneno yake. Anamwuliza Ayubu kuhusu mashtaka yake juu ya ukosefu wa haki ya Mungu. Je, bado anataka kusema kwamba Mungu amekosa ili athibitishe kwamba

yeye hana hatia? Ayubu anataka kuwa sawa na Mungu, kuchukua sehemu yake na kutawala kanuni za haki ya ulimwengu badala yake, ili aamue yaliyo sawa na yaliyo mabaya (6-9)? Ikiwa hivyo, Ayubu avae nguo za heshima za Mungu na akae katika mahakama ya waovu wote wenye kiburi. Ndipo Mungu atakubali makadirio ya Ayubu kuhusu nafsi yake kuwa sawa (10-14).

Wanyama wawili (40:15-41:34)

Kabla Ayubu hajapokea mwaliko wa Mungu kutawala kanuni za haki, Mungu anamwonya kwamba kazi hiyo ingekuwa ngumu sana kuliko kutawala kanuni za kawaida za viumbe. Kwa hiyo inafaa azingatie kwanza ana mamlaka gani, kwa mfano juu ya wanyama. Mifano miwili inatosha kumwonyesha kwamba hana uwezo wo wote juu ya mambo hayo. Mfano wa kwanza ni kiboko. Ni mmojawapo wa viumbe vikubwa na vyenye nguvu vilivyoumbwa na Mungu (15-18), ana nguvu sana katika nchi kavu, na majini hana shida, tena ni vigumu sana kumkamata (19-24).

Mnyama wa pili ambaye Ayubu anaonyeshwa ni mamba mkubwa. Je, anaweza kumvua kwa ndoana kama vile anavyovua samaki? Anaweza kumfundisha kusema, kufanya kazi au kumfuga kama mnyama wa kuchezea watoto? Anaweza kumwuza sokoni (41:1-6)? Hata angeweza kumkamata mmojawao, angesikitika tu. Asingependa kumkamata wa pili (7-8)! Kwa hiyo, iwapo mtu mwenye akili yake timamu hathubutu kumchokoza mamba, haiwezekani kabisa hata kufikiri kusimama na kumchokoza Mungu (9-11).

Kisha Mungu anaeleza maumbo ya kutisha ya mnyama yule anayefanana na joka lenye magamba: Ngozi yake ya magamba kama silaha za vita, nguvu kubwa ya kinywa chake na meno yake ya kutisha (12-17). Akipuliza hewa na maji kutoka puani, inaonekana kama anapuliza moto na moshi (18-21). Mnyama huyo ana nguvu za kutisha, hata mtu mwenye nguvu anaweza kutishwa akitazama anavyocheza (22-25). Hakuna silaha inayoweza kupenya katika magamba yake yanayofanana na chuma (26-29). Akisogea kutoka nchi kavu na kuingia majini, anachimba matope kama chombo cha kupuria nafaka na kuvuruga maji hata povu lionekane nyuma yake (30-32). Kiumbe kile cha kutisha ni mfalme wa wanyama. Hashindwi na wanadamu, lakini hata hivyo ni sehemu ya ulimwengu ambao Mungu aliumba (33-34).

Ayubu ajikabidhi kwa Mungu (42:1-6)

Ingawa Ayubu hajapata jibu kwa matatizo yake, lakini anajua kwamba Mungu analo jibu hilo, naye hatakosa. Mungu hakumpa Ayubu sababu nyingi kwa shida zake, lakini alimpa ujuzi zaidi kuhusu Mungu mwenye nguvu na uwezo wote, na jambo hili lilibadilisha mawazo ya Ayubu.

Wakati huo Ayubu anaona kwamba Mungu ni juu ya mambo yote naye anatawala yote. Anaangalia hata mambo madogo sana. Ingawa Ayubu labda haelewi makusudi ya Mungu yanayomsababisha kufanya mambo mengine, lakini ana uhakika kwamba anafanya mambo yote kadiri ya makusudi yake Mwenyewe, na makusudi yake yamekamilika. Ayubu ameshindwa, lakini vile vile amepata amani, kwa sababu Mungu aliyejidhihirisha kwake ni mkuu kuliko yeye alivyoweza kuhisi. Haendelei kudai kitu kwa Mungu, bali anamwabudu tu (42:1-2).

Kwa unyenyekevu anakiri kwamba, mashtaka ya Mungu juu yake ya kuwa 'ametia mashauri giza kwa maneno yasiyo na maarifa' yalikuwa kweli (3, taz.38:2). Mungu alimwita ajibu maswali yake (4, taz.38:3), lakini wakati huo hana la kusema. Hapo awali alikuwa na ujuzi kuhusu Mungu kwa kusikia kwa watu wengine tu, lakini wakati huo yeye mwenyewe amekutana na Mungu. Ingawa maswali yake hayakujibiwa, Ayubu ameridhika kabisa (5-6). Inawezekana kwamba kwa matatizo mengine ya maisha hatupati jibu, lakini tukijikabidhi kwa Mungu kabisa, hatuna haja ya kupata jibu, bali tutaishi katika amani yake.

Mungu amwinua Ayubu (42:7-17) Marafiki watatu, ingawa katika hotuba zao kulikuwa na ukweli, wakati huo wanaelezwa kuwa wamekosa. Ayubu, ingawa alitumia maneno makali na kulalamika isivyostahili, wakati huo anatangazwa kuwa hakukosa. Kwa kumtuhumu Ayubu kwamba alikuwa na dhambi nyingi, marafiki watatu hawakusema ukweli, lakini Ayubu alipojidai kuwa mnyofu bila dhambi kubwa, wakati huo anathibitishwa kuwa na ukweli. Maneno ya marafiki kwamba mateso siku zote ni matokeo ya dhambi za mtu binafsi, yanaonyeshwa kuwa ni kinyume, ambapo hamu kubwa ya Ayubu ya kukutana na Mungu mwenye haki imetimizwa. Marafiki walitegemea mapokeo ya mila tu, lakini Ayubu alitafuta ukweli. Marafiki walisema habari za Mungu tu, ambapo Ayubu alisema naye Mwenyewe (7-8).

Ayubu hakuwa na kiburi katika ushindi wake, wala marafiki hawakuwa na uchungu kwa kushindwa kwao. Ayubu aliwaombea marafiki zake, nao kwa unyenyekevu wao, walimwomba Mungu

awasamehe, wakimtolea sadaka (9).

Inavyoonekana, hata wakati huo Ayubu hakujua (na labda hakujua wakati wo wote) kwamba sababu kuu ya mateso yake ilitokana na mashtaka ya Elifazi aliyoyapeleka mbele ya Mungu (taz.l:ll; 2:5). Wakati huo ambapo Elifazi ameonekana kuwa amekosa, ilikuwa haki tu kwamba mali na furaha ya kifamilia ya Ayubu ya hapo awali virudishwe kwake. Wakati huo huo ulikuwa pale alipowaombea wale waliomlaumu. jambo hili liliwaonyesha wenyeji wenzake kwa Ugonjwa wake ulipona, afya njema ilimrudia, watoto njia ya pekee waliyoweza kuielewa kwamba walizaliwa badala ya wale waliokufa, na mali yake Mungu alipendezwa na Ayubu. Wakati ambao iliongezeka maradufu kuliko ile ya siku za kwanza mambo yote yalibadilika katika mateso ya Ayubu (10-17).